# MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA



JARIDA LA HALI YA HEWA KILIMO

*Na.20. Msimu wa Kilimo 2022/23* *Tathmini ya Aprili 11-20, 2023 na Matazamio kwa Kipindi cha Aprili 21-30, 2023*


**MUHTASARI**

- Unyevunyevu katika udongo unatarajiwa kuongezeka kutokana na mvua zinazoendelea.
- Unyevu mwingi wa udongo unaweza kuzorotesha shughuli za kilimo, ukuaji na maendeleo ya mazao kutokana na mashamba kujaa maji.
- Wakulima, wafugaji na wavuvi wanashauriwa kupata ushauri wa maafisa ugani na kutumia taarifa za hali ya hewa katika shughuli zao za kila siku.

## MIFUMO YA HALI YA HEWA KATIKA KIPINDI CHA APRILI 11-20, 2023


Katika dekadi hii, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) haikuwa na mabadiliko wakati ile iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) ilipungua nguvu. Hali hii iliruhusu ukanda mvua (ITCZ) kusalia katika maeneo ya kaskazini mwa nchi.

Joto la bahari katika eneo la kusini magharibi mwa bahari ya Hindi lilikua la juu ya wastani hali iliyopelekea hewa yenye unyevunyevu kuvuma kutokea baharini kuelekea ukanda wa pwani. Joto la bahari la eneo la tropiki ya kati ya bahari ya Pacific lilikua la wastani.

Joto la bahari la mashariki mwa bahari ya Atlantic (pwani ya Angola) lilikua la juu ya wastani na kuwa na mchango hafifu katika kusafirisha upepo wenye unyevunyevu kutoka misitu ya Congo kuelekea maeneo ya magharibi mwa nchi

## TATHMINI YA MVUA KATIKA KIPINDI CHA APRILI 11-20, 2023

Maeneo mengi ya nyanda za juu kaskazini mashariki na mikoa ya kati yalipata kiwango kidogo cha mvua kisichozidi jumla ya 50 mm katika siku kumi. Kwa upande mwingine, maeneo mengi ya ukanda wa kusini (pamoja na kusini mwa Morogoro), pwani ya kaskazini, na visiwa vya Unguja na Pemba yalipata mvua nyingi zaidi ya milimita 50, na maeneo machache kiasi cha 100 mm hadi 150 mm za mvua. Kiasi kikubwa zaidi cha mvua (zaidi ya milimita 200) ilinyesha katika maeneo machache ya kusini mwa mkoa wa Morogoro kama inavyooneshwa katika Kielelezo.




Kielelezo: Kiasi cha mvua katika kipindi cha Aprili 11-20, 2023

## TATHMINI YA HALI YA KILIMO KATIKA KIPINDI CHA APRILI 11-20, 2023

Mvua zilizonyesha katika dekadi hii, zimesaidia ukuaji wa mazao katika maeneo yanayopata mvua masika na Msimu.

Maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka hususan mikoa ya Njombe, Iringa, Mbeya, Ruvuma, Rukwa, Tabora na Kigoma, mahindi yalikuwa katika hatua ya kukomaa.

Aidha, zao la mahindi katika maeneo yanayopata mvua za masika yapo katika hatua ya kati ya jani la tatu na la tisa, na wakulima wameendelea na palizi.

Zao la mpunga lipo katika hatua ya kuchanua katika maeneo ya mikoa ya Morogoro kusini, Tabora, Mbeya na

Rukwa.
Wakulima katika mikoa ya Iringa, Njombe na Mbeya na wanamalizia kuvuna zao la viazi mviringo.
Upatikanaji wa maji na malisho kwa ajili ya mifugo ulikuwa wa kuridhisha katika maeneo mengi nchini kutokana na mvua zinazoendelea.

## HALI YA MAJI KATIKA KIPINDI CHA APRILI 11-20, 2023

Kwa ujumla kina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji kwenye mito na mabonde kiliongezeka kutokana na mvua zilizonyesha isipokuwa maeneo ya mikoa ya kati ambapo kulikuwa na mvua chache.

## MIFUMO YA HALI YA HEWA INAYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA APRILI 21-30, 2023

Katika dekadi hii, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kusini mwa dunia inatarajiwa kuwa na mabadiliko kidogo wakati ile iliyopo kaskazini mwa dunia inatarajiwa kupungua nguvu. Hali hii inatarajiwa kuruhusu ukanda mvua (ITCZ) kuendelea kusalia katika maeneo yaliyoko kaskazini mwa nchi.
Joto la bahari katika eneo la kusini magharibi mwa bahari ya Hindi linatarajiwa kuwa la juu ya wastani hivyo kuendelea kuruhusu upepo wenye unyevunyevu kuvuma kutoka baharini kuelekea maeneo ya pwani ya nchi. Katika eneo la tropiki ya kati ya bahari ya Pacific joto la bahari linatarajiwa kuwa la juu ya wastani ambalo litasaidia kuimarisha mifumo ya mvua katika baadhi ya maeneo nchini.
Kwa upande mwingine, joto la bahari mashariki mwa bahari ya Atlantic (pwani ya Angola) linatarajiwa kuwa la juu ya wastani na hivyo kuwa na mchango hafifu katika kusafirisha upepo wenye unyevunyevu kuvuma kutoka misitu ya Congo kuelekea maeneo ya magharibi mwa nchi.

## HALI YA HEWA INAYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA APRILI 21-30, 2023

Maeneo ya kanda ya Ziwa Viktoria (mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara), nyanda za juu kaskazini mashariki (mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro) na magharibi mwa nchi (mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora) yanatarajiwa kupata mvua na ngurumo za radi katika maeneo machache.

Pwani ya kaskazini (mikoa ya Tanga, maeneo ya kaskazini mwa Morogoro, Pwani na Dar es Salaam pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba), nyanda za juu kusini magharibi (mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa), pwani ya kusini (mikoa ya Mtwara na Lindi), na kanda ya kusini (mkoa wa Ruvuma na maeneo ya kusini mwa Morogoro) zinatarajiwa kupata mvua na ngurumo za radi kwa baadhi ya maeneo.

Kanda ya kati (mikoa ya Dodoma na Singida) inatarajiwa kupata mvua zinazoambatana na ngurumo za radi katika maeneo machache.

## HALI YA HEWA KILIMO: MATARAJIO NA USHAURI KATIKA KIPINDI CHA APRILI 21-30, 2023

Mvua zinazotarajiwa katika maeneo mengi nchini zitaongeza unyevunyevu kwenye udongo ambao utaendelea kusaidia ukuaji na maendeleo ya mazao, ingawa unyevu wa udongo mwingi na wa kupitiliza unaweza kuzorotesha shughuli za kilimo, ukuaji na maendeleo ya mimea kutokana na kujaa maji shambani.

Wakulima na maafisa ugani wanashauriwa kuendelea kufuatilia kwa ukaribu hali ya mazao na mashamba ili kuweza kukabiliana na athari zinazoweza kutokana na unyevu wa udongo wa kupitiliza na milipuko ya wadudu waharibifu na magonjwa ya mimea pale vitakapojitokeza.

Jamii za wavuvi wanashauriwa kuendelea kufuatilia taarifa za hali ya hewa za kila siku, hususan kwenye baharini ya Hindi na maziwa makuu ili kufanya maamuzi juu ya wakati sahihi wa kwenda kufanya shughuli za uvuvi. Wafugaji pia wanashauriwa kuhakikisha mifugo yao inalindwa dhidi ya hali mbaya ya hewa na magonjwa ya mlipuko.

Kwa ujumla, inashauriwa kuzingatia utabiri wa hali ya hewa katika shughuli na mipango ya kila siku.

## HALI YA MAJI INAYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA APRILI 21-30, 2023

Kina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji kwenye mito kinatarajiwa kuongezeka kutokana na mvua zinazotarajiwa.
Hata hivyo, jamii inashauriwa kuvuna maji ya mvua kwa ajili ya matumizi ya baadae.



Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, Chuo Kikuu cha Dodoma,
1 Mtaa wa CIVE, S.L.P 27, 41218 Dodoma, Simu: +255 26 2962610, Nukushi: +255 26 2962610,
Barua pepe: met@meteo.go.tz; agromet@meteo.go.tz; Tovuti: *www.meteo.go.tz*
(ISO 9001:2015 Certified in Aviation Services)